

TANGAZO LA SERIKALI Na. 148 la tarehe 8/3/2024

SHERIA YA MAJINA YA BIASHARA,  
(SURA YA 213)

**KANUNI**

(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 22)

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UMILIKI MANUFAA ZA MWAKA 2024

Jina  
T.S. Na.  
714 la 2023

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Umiliki Manufaa za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Umiliki Manufaa za Mwaka 2023 ambazo katika Kanuni hizi zitarejewa kama “Kanuni kuu”.

Marekebisho  
ya kanuni ya 9  
kwa-

2. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 9

(a) kufuta maneno “kuhusu uamuzi huo” yanayoonekana katika kanuni ndogo ya (2) na badala yake kuweka maneno “sababu za uamuzi huo ndani ya siku tatu tangu tarehe ya uamuzi”.

(b) kuongeza baada ya kanuni ndogo ya (2) kanuni ndogo ifuatayo:

“(3) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa Msajili chini ya kanuni hii anaweza kukata rufaa kwa maandishi kwa Waziri ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya uamuzi huo akibainisha sababu za rufaa na uamuzi wa Waziri utakuwa wa mwisho.”

Dodoma,  
16 Februari, 2024

ASHATU K. KIJAJI  
Waziri wa Viwanda na Biashara